



# **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

### **KUAHIRISHA KAMPENI ZA UBUNGE JIMBO LA HANDENI MJINI**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inautangazia Umma kuwa kufuatia kifo cha Mgombea Ubunge Jimbo la Handeni Mjini kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi ( CCM) Dr. Abdallh O. Kigoda, shughuli za kampeni za Uchaguzi wa Bunge zimesitishwa katika Jimbo hilo.

Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 37 na 49 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi sura ya 343 ya mwaka 1985.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza ratiba ya tarehe ya Uteuzi wa Mgombea mwingine toka Chama cha Mapinduzi (CCM). Tarehe ya kuanza upya kwa kampeni na tarehe ya Uchaguzi wa Bunge katika Jimbo la Handeni Mjini. Kampeni nyingine za Urais na Udiwani zitaendelea kama kawaida.

Kailima R. Kombwey

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**